



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



**TAARIFA KWA WATOA HUDUMA ZA AFYA WANAHUDUMIA  
WANACHAMA WA NHIF KUHUSU UHAKIKI WA WANACHAMA KWA  
NJIA YA ALAMA ZA KIBAOLOGIA**

*Desemba 1, 2023*

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unaendelea kuimarisha mfumo wake wa uhakiki wa wanufaika wake katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanufaika wanaostahili wanapata huduma bora za matibabu kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizowekwa kwa watoa huduma wake. Katika kutekeleza dhamira hiyo, Mfuko unapenda **kuwakumbusha Watoa huduma kurejea mawasiliano yaliyofanyika tarehe 31 Agosti, 2023 kwa barua yenye Kumb. Na. EA.135/317/01-A/102** kuhusu suala hili kama ifuatavyo:-

1. Mfuko kwa kushirikiana na Watoa huduma unaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA kwa **kutumia alama za vidole na sura kuhakiki wanufaika wake ili ifikapo tarehe 1 Januari, 2024** vituo vyote viweze kuhakiki kwa utaratibu huo.
2. Hivyo, Watoa huduma wote wanakumbushwa kuhakikisha wanakuwa na vifaa hivyo (biometric and facial recognition gadgets) kabla ya tarehe 31 Disemba, 2023 kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa awali.
3. Baada ya tarehe hiyo, malipo yote ya madai ya Watoa huduma yatafanywa kwa kuzingatia wanachama waliohakikiwa vituoni kwa kutumia alama za vidole au sura kama inavyokusudiwa na si vinginevyo.
4. Kwa sasa Mfuko unaendelea kufanya zoezi la uunganishaji wa vifaa hivyo kwa Watoa huduma ambao tayari wamevinunua na kutoa taarifa katika Ofisi za Mfuko za mikoa na Zanzibar.

Mfuko unaendelea kuhimiza ushirikiano katika hili na kwa ufafanuzi au maelezo zaidi tafadhali Mtoa huduma awasiliane na Uongozi wa Ofisi ya NHIF ya mkoa husika au Ofisi ya Zanzibar.

Imetolewa na;

Anjela A. Mziray  
**MENEJA UHUSIANO**